

KATIKA UWEPO WAKE



Asante, Ndugu Neville, Bwana akubariki kwa wengi sana.

Na habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa makuu kurudi hapa kwenye jengo hili tena usiku wa leo, na kuuhihi Uwepo usioshindwa wa Bwana wetu, kama vile Yeye alivyotoa ahadi. Na sasa, ninajua ya kwamba wengi wenu mmeekaa huku kwa ajili ya Ujumbe mfupi usiku wa leo, jambo ambalo ninashukuru sana. Na wengi wenu ingali itawabidi kuendesha magari mbali usiku wa leo, kwenda nyumbani. Wengine mmeshaachilia moteli zenu, ninavyofahamu. Nasi tutajaribu kutowakalisha sana, kwa hiyo hiyo ndiyo sababu tumekuja mapema kusudi tuweze kuondoka mapema.

² Na sasa tutaninii, mara niwezapo tu, nitatangaza wakati ambapo huenda tutaanza, nimepigiwa simu kadhaa alasiri ya leo, kujua wakati tutakapoanza kuhusu vitabu hivi, ama masomo haya. Nami nafikiri, Bwana akipenda, ninataka kuchukua, wakati ujao tutakapoanza, juu ya ile Mihuri Saba ya Ufunuo, na ile mihuri saba ya kawaida. Na, basi kama tukiwahi, tuchukue ile mihuri saba upande wa nyuma wa Kitabu hicho, mnaona. Sasa, hilo linaweza kuchukua wakati mfupi. Unaona, ipo mihuri saba ambayo imefunguliwa; kuna mapigo saba, baragumu saba, saba hizo zote; na hiyo mihuri tungeweza kuichukua kwanza. Lakini basi upande wa nyuma wa Kitabu hicho umetiwa muhuri kwa mihuri saba. Danieli alizisikia sauti, ngurumo, na akakatazwa kuziandika. Yohana alikatazwa kuziandika. Bali ilitiwa muhuri upande wa nyuma wa Kitabu, hiyo ni kusema, baada ya siri zote za Kitabu kutolewa na kufunuliwa. Mnaona Danieli alisema pale, “Siri hizo katika siku za sauti hizi, siri ya Mungu inapaswa kufunuliwa ifikiapo kwenye wakati huo.” Mnaona, “hiyo siri,” kwamba Mungu ni nani, jinsi alivyofanyika mwili, mambo yote haya yanapaswa kufunuliwa kwenye wakati huo. Na tena ndipo—ndipo tuko tayari kwa ajili ya ile Mihuri Saba upande wa nyuma wa Kitabu, ambayo hata haijafunuliwa kwa mwanadamu, hata haijaandikwa katika Biblia, bali italazimu ilingane kikamilifu na Biblia yote, nami nafikiri litakuwa ni jambo kubwa.

³ Kwa hiyo sasa tutajaribu kuharakisha tupate kumaliza. Nawashukuru kila mmoja wenu kwa wema wenu na uwepo wenu, na—na yote mliyofanya, tunawashukuru sana. Na sasa na—natumaini ya kwamba hatutawaweka kwa muda mrefu sana usiku wa leo, kwa sababu ninyi ni wavumilivu sana kuketi, kusimama. Mke wangu alisema huko nyuma, alikuwa akizungumza kuhusu jana usiku, akasema, “Niliwaona wanawake ambao kwa namna fulani hata walikuwa ni wanene,

wakisimama pale, na nguo zao zimelowa jasho, wamesimama pale, wakishikilia tu kwa dhati kila Neno.” Hiyo ndiyo sababu ninapenda kukaa chini ya upako wa Roho Mtakatifu, ili kwamba wakati unapotoka unawaambia watu Ukweli mtupu, unaona, wala si kitu ila ni Ukweli. Ndipo basi wanaweza kushikilia jambo Hilo na litakuwa ni sawa.

⁴ Sasa ninataka kuwaomba msamaha wenu kwa dakika chache. Niliondoka mapema kidogo asubuhi ya leo. Na kanda zimezimwa wakati huu, nami—nami katika dakika moja nitawaambia wenye kurekodi wakati watakapokifungulia kinasasauti. Ninataka kumalizia *Kuhesabu Kinyumenyume*, dakika tano kwa huo, kabla sijaondoka. Nilisahau na kwenda zangu, niliendelea tu asubuhi ya leo hata nikaondoka tu bila ya kusema jambo lolote kuuhusu. Lakini, kwa namna fulani niliwaachia, “Kuhesabu kinyumenyume kulikuwa ni nini?” Mnaona? Ninajua tuko katika kuhesabu kinyumenyume, lakini kuhesabu kinyumenyume ni kitu gani? Mnaona? Kama hamjui kuhesabu kinyumenyume ni nini, basi kwa namna fulani mtachanganyikiwa. Na kwa hiyo ni—ningetaka ku—kuumalizia huo, kuninii tu, na kujaribu kuwa katika sauti ile ile niliyokuwu nayo kumalizia kanda hii sasa, ili kanda hiyo ipate kutolewa, *Kuhesabu Kinyumenyume*. Sasa ninyi nyote mtaniwia radhi kidogo tu, basi ninataka kukamilisha kanda hiyo. Je! mtaniwia radhi kwa muda mfupi, kisha tutaanza huo mwingine? [Kusanyiko linasema “Amina.”—Mh.] Na sasa—sasa mnaorekodi kanda, mkipenda, fungulieni kinasasauti chenu sasa.

[Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu Branham anaelezea katika aya ya 4-5 ya kwamba aliingiza sehemu hii isiyokuwapo katika ujumbe wake wa asubuhi uitwao *Kuhesabu Kinyumenyume*, kama aya ya 106-111—Mh.]

⁵ Tumekuja tu kutoka sehemu mbalimbali, na tumekuwa na wakati mzuri sana katika jumbe tatu zilizopita, zilizozungumzia juu ya somo la—la mafundisho mbalimbali na kadhalika ambazo tumezitao. Ninakumbuka tu kwenye wakati huu inanibidi kutoa nafasi ndogo mle ndani, ninyi watu kwenye kanda, mpate kuzibadilisha kanda zenu. Nitawaambia nitakapokuwa tayari mzifungulie. Vema. Sasa, inanibidi kuangalia jambo hili. Inaonekana kana kwamba ni kitu cha kawaida, bali hao vijana inawabidi kuipata kanda hiyo. Nao hawawezi kukiborongea kabisa; wakifanya hivyo, watu walio huko nje hawataielewa. Kwa hiyo inatubidi tuichukue kwa jinsi hii. Na kama mtu fulani atatoka tu kwenye hicho chumba na kuniashiria pale, Junior, wakati wakiwa tayari kuzibadilisha kanda. Asanteni sana, ninyi watu, ninasema tena, kwa ajili ya wema wenu na kila kitu. Vema, tuko tayari sasa, mnaweza kuvifungulia.

⁶ Bwana awabariki. Tuna furaha kuwa hapa maskanini tena usiku wa leo. Mahali hapa pamejaa watu huku watu wengi

wamesimama kote usiku wa leo tena, kwenye siku tatu za . . . ama nyakati tatu za ibada. Ningetamani kwamba kama mtu ye yeyote akiisikiliza kanda hii, kwamba wangetaka kurudi na wachukue kanda ya jana usiku. Mwitafakari nyumbani mwenu. Ni ninii—ni kiwango cha sasa cha huduma ambayo Bwana amenipa. Hasa ningetaka wahudumu kuisikia hiyo kabla sijayatembelea makanisa yao na kuja manyumbani mwao. Sasa ningewataka wao ku—kuipata hiyo. Sasa, asubuhi ya leo tulizungumza juu ya somo la *Kuhesabu Kinyumenyume*, Kanisa likiwa tayari kuondoka.

⁷ Na sasa usiku wa leo, Mungu akipenda, tunazungumza juu ya somo la *Katika Uwepo Wake*. Na, loo, jinsi tunavyomshukuru Mungu kwa majaliwa kwamba tunaweza kuja katika Uwepo Wake. Lakini, kwanza, ningewataka ninyi nyote mfungue kwenye Biblia zenu pamoja nami kwa nabii Isaya, mlango wa 6 wa nabii Isaya. Sote tunajua ya kwamba Isaya alikuwa ni nabii mkuu, na mmoja wa manabii wakuu wa siku zake. Alimalizia maisha yake kwa kupasuliwa na misumeno, kwa ajili ya ushuhuda, kama mfia imani kwa nguvu za Mwenyezi Mungu. Katika Kitabu cha Isaya, mlango wa 6, ninaanzia kwenye kifungu cha 5, kusoma. “Ndipo niliposema, ‘Ole wangu!’ Kwa maana . . .” Labda nianze na kifungu cha 1. Hebu samahani kidogo. Hebu tuanzie kwenye kifungu cha 1 na kuendelea kusoma mpaka karibu kifungu cha 8.

Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nilimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu.

Juu yake walisimama maserafi; kila mmoja akiwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.

Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni BWANA wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake.

Na misingi ya vizingiti ikatikisika kwa sababu ya sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi.

Ndipo niliposema, Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, BWANA wa majeshi.

Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia; naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu;

Akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako, na uovu wako umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa.

Kisha nikaisikia sauti ya Bwana akisema, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi.

⁸ Bwana na alibariki Neno Lake. Ninafikiri hilo ni Andiko la kustaajabisha sana. Tunaona ya kwamba, kwenye Uwepo wa Mungu, wanadamu hujitambua kuwa ni wenyewe dhambi. Tunaweza kujisikia wazuri sana tunapokuwa huko nje mahali mbalimbali, na kujisikia kana kwamba sisi ni watu wazuri sana, bali tukipata kuingia katika Uwepo wa Mungu, basi tunaona jinsi tulivyo wadogo.

⁹ Nikisimama si muda mrefu uliopita pamoja na ra—rafiki yangu ambaye nilikuwa na majaliwa ya kumwongoza kwa Kristo, Bert Call, huko New Hampshire, mwindaji mwenzangu, tulikuwa tumesimama karibu na Maporomoko ya Cold Brook huko Adirondack, na yalikuwa ni maporomoko makubwa mnno. Niliipeleka familia yangu mwaka uliopita huko juu kuyaangalia. Huko nyuma kabisa kando ya barabara, inakubidi kwenda kwa miguu kuyafikia. Na wakati tulipoona hayo maji ya bluu-kijani kibichi yakitiririka kwa nguvu nyingi sana kutoka milimani, na kufoka juu ya miamba, Bert alisimama pale na kuniangalia, kisha akasema, “Salala, Billy, inamfanya mwanadamu kujisikia mdogo sana,” akapima kama robo ya nchi ya vidole vyake. Nami nikasema, “Hiyo ni kweli, Bert.” Sasa, hayo ndiyo yote aliyojua ya kuingia katika Uwepo wa Mungu, kuona uumbaji Wake.

¹⁰ Ninamshangaa yule mtu aliyeandika *Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu*, kama hakuangalia juu usiku mmoja na kuziangalia nyota, jinsi zilivyo mbali! Miezi michache iliyopita, mimi, Ndugu Fred, na Ndugu Woods, tulikuwa tumesimama pamoja na Ndugu Mc Anally huko nje kwenye jangwa la Arizona, tulikuwa tukipima, tukijaribu, nyota moja, jinsi ilivyokuwa karibu na nyingine. Na huku zikiwa kwenye umbali wa mamilioni na mabilioni ya maili, hazikuonekana kuwa zaidi ya robo inchi kutoka moja mpaka nyingine. Ndipo tukaanza kuwazia, kulingana na thibitisho la sayansi la jambo hilo, nyota hizo labda ziko mbali sana moja kutoka nyingine kuliko tulivyo kutoka ziliko. Mnaona jinsi ilivyo?

¹¹ Ndipo tunatambua jinsi tulivyo wadogo tunapotambua jinsi Yeye alivyo mkuu, na jinsi tunavyokaribia katika kuja katika Uwepo Wake. Kwa njia moja ama nyingine, daima limeleta ushawishi mkubwa sana kwa watu kuja katika Uwepo wa Mungu. Nimeona wakati katika huduma yangu ambapo ungeuona Uwepo wa Mungu ukishuka ukaingia katika mahali ambapo hata ungemleta mtu huku na kuwafunulia tu maisha yao, na kutaja dhambi zao za kila namna ya matendo machafu, nao unasababisha kimya kitakatifu sana juu ya watu hata wanaondoka kwenye mstari wa maombi kabla hawajakuja kuombewa, na kukimbia madhabahuni na kujiweka sawa na

Mungu kabla hawajakuja katika Uwepo Wake. Unaona, kuna jambo kuhusu kuja katika Uwepo wa Mungu, linayafanya mambo kutokeea. Nimewaona watu wamelala kwenye vitanda vya wagonjwa na machela.

¹² Usiku ule huko chini Meksiko, wakati yule mtoto mchanga aliyekufa alikuwa amelala chini ya blanketi, ambaye aliletwa na maskini yule mama wa Kihispaniola, ama mama mdogo wa Kimeksiko, hasa, aliyemleta. Wakati walipoona, maelfu kadhaa ya hao watu walioona, labda elfu hamsini ama sabini na tano kwenye kusanyiko moja, walipomwona maskini mtoto huyo mdogo aliyekufa akifufuka, wanawake walizimia, watu walitupa mikono yao juu na kupiga makelele. Kwa nini? Walitambua ya kwamba mwanadamu asingeweza kufanya jambo hilo, kwamba walikuwa katika Uwepo wa Mwenyezi Mungu. Na ilisababisha jambo fulani kutukia.

¹³ Nimekuwa na majaliwa ya kuwasikia watu wacha Mungu wakihubiri. Ilisemwa wakati mmoja juu ya Charles Finney, maskini mtu mdogo, kamwe hakuwa na uzito wa zaidi ya karibu pauni mia moja na kumi, lakini alikuwa na njia ya kuzungumza kwa nguvu sana mpaka... Alikuwa akijaribu kusikika kwa sauti siku moja kwenye jengo moja. Hawakuwa na mfumo wa Vipaza Sauti wakati huo. Basi kulikuwako na mtu aliyekuwa akikarabati, huko juu kwenye roshani, ama huko juu kwenye paa la mahali hapo, naye akasikia mtu huyo akiingia, kwa hiyo hakujuu hao walikuwa ni akina nani, alinyamaza tu kimya. Na Bw. Finney alikuwa akienda kujaribu kusikika kwa sauti. Baada ya kutumia wakati mwingu katika maombi kwa ajili ya uamsho huo ambao alikuwa akienda kuufanya, alijaribu sauti yake aone jinsi ingesikika. Aliingia upesi mimbarani, na kusema, "Tubu, la sivyo utaangamia!" Naye alilisema kwa nguvu sana—nguvu, baada ya kuwa chini ya upako wa Mungu, mpaka mtu huyo akaanguka kutoka juu ya roshani, mpaka chini sakafuni, ama, kutoka juu ya jengo hilo, akaanguka sakafuni.

¹⁴ Alihubiri Injili hivi kwamba mpaka alisimama huko Boston, Massachusetts, kwenye dirisha ghuba dogo, kwa kuwa hapakuwapo na kanisa lingaliweza kuenea umati wake. Naye alisimama hapo kwa nguvu nyingi sana, na kuhubiri kuzimu jinsi kulivyo, mpaka wafanyakazi wakiwa wameshika vikapu vyao chini ya mikono yao, walianguka barabarani na kupaza sauti wapate rehema. Katika Uwepo wa Mungu! Wahubiri wakuu ambao wameweza, kwa Neno la Mungu, kuuleta Uwepo wa Mungu kwa wasikilizaji. Na iwe mbali na mtu kwamba miyo yao ingefanywa kuwa migumu sana hata wasiweze kamwe kutambua Uwepo wa Mungu. Na likae mbali!

¹⁵ Wakati mtu wa kwanza, mara alipotenda dhambi na kufanya kosa, na wakati Mungu alipokuja katika uwepo wake, ama, ye ye alipoingia kwenye Uwepo wa Mungu, "Adamu," asingeweza

kusimama katika Uwepo wa Mungu. Alikimbia akajificha kichakani na kujaribu kujifunika kwa jani la mtini, kwa sababu alikuwa amesimama katika Uwepo wa Yehova, Muumbaji. Hivyo ndivyo alivyolichukulia yule mtu wa kwanza, baada ya yeze kufanya dhambi na kujaribu kuingia katika Uwepo wa Mungu akiwa na dhambi nafsini mwake. Asingeweza kujificha, kwa sababu alikuwa bado ni mchanga. Dhambi haikuwa imeshika kama vile ambavyo imeota mizizi miyoni mwa watu siku hizi, bali alitambua vizuri sana ya kwamba alikuwa amesimama mbele ya Muumba wake. Sasa, yeze alijificha vichakani wala asingetoka, wala asingetoka mpaka Mungu alipofanya maandalizi kwa ajili yake.

¹⁶ Tungeweza kurudi nyuma, na kuchukua Mwanzo mlango wa 17 na kifungu cha 3, wakati yule mzee mashuhuri, Ibrahimu, wakati alipoingia katika Uwepo wa Mungu, na Mungu akasema naye (katika mlango wa 17) katika Jina la Mwenyezi Mungu, Ibrahimu alianguka kifudifudi. Yule mzee mashuhuri, mtumishi wa Mungu, asingeweza kusimama katika Uwepo wa Mungu, ingawa alikuwa amemtumikia kwa muda wa miaka ishirini na mitano, kwa uaminifu. Lakini wakati Mungu alipokuja mbele zake, mzee huyo alianguka kifudifudi kwa sababu asingeweza kusimama katika Uwepo wa Mungu.

¹⁷ Katika Kutoka 3, tunaona ya kwamba Musa, yule mtumishi mkuu na nabii wa Mungu, wakati alipokuwa huko upande wa nyuma ndani kabisa ya jangwa, mtu huyo alikuwa ni mtu mtakatifu. Alikuwa amezaliwa kwa kusudi hilo. Alizaliwa tangu tumboni mwa mama yake awe nabii. Alikuwa amejaribu kupata elimu yake na kufanya kila alichoweweza kufanya kuwakomboa watu wake, kwa sababu alifahamu kuwa alipaswa kuwakomboa watu wake, bali ni wakati alipokuwa amelifahamu kwa msimamo wa kitheolojia. Alikuwa amefunzwa. Alikuwa ameelimika sawasawa. Angaliweza kuwafundisha Wamisri hekima, ambao walikuwa ndio watu werevu kuliko wote duniani. Alijua yote ndani na nje. Aliyafahamu Maandiko kutoka A mpaka Z. Alizijua ahadi ambazo Mungu alikuwa amefanya. Alizijua kutoka kwenye msimamo wa kiakili. Naye alikuwa ni m—mwanajeshi mkuu. Lakini siku moja upande wa nyuma ya jangwa, wakati alipoingia katika Uwepo wa Mungu, alivivua viatu vyake upesi na—na kupiga magoti, akiuju ya kwamba alikuwa katika mahali patakatifu. Asingeweza kusimama kwa miguu yake wakati alipokuja katika Uwepo wa Mungu, alianguka kifudifudi kama vile Ibrahimu alivyofanya. Asingeweza kusimama katika Uwepo wa Mungu.

¹⁸ Katika Kutoka 19:19, wakati watu wa Mungu waliochaguliwa tangu huko nyuma katika siku za Ibrahimu, kutoka Ibrahimu akaja Isaka, Isaka akaja Yakobo, kutoka kwa Yakobo wakaja wale wazee wetu, na miaka baada ya miaka ilikuwa imewakuza watu watakatifu, watu mashuhuri,

watu waliochaguliwa, jamii iliyochaguliwa, iliyotakaswa, watu watakatifu, nao walikuwa wamemtumikia Mungu maishani mwao. Ndipo siku moja Mungu akasema, "Wakusanyeni Israeli hapa, nitasema nao."

¹⁹ Lakini wakati Mungu aliposhuka juu ya Mlima Sinai, na mlima wote ukashika moto, nao moshi ulikuwa ukifoka ukitoka humo kama tanuru, na Sauti ya Mungu ikanguruma. Israeli walianguka kifudifudi na kusema, "Hebu Musa aseme, wala si Mungu, tusije tukafa." Mwanadamu, katika Uwepo wa Mungu, hutambua ya kwamba ye ye ni mwenye dhambi! Hata hivyo wao walikuwa, kila mmoja, ametahiriwa kulingana na Torati. Walikuwa wametimiza amri na kila kitu, bali wakati Mungu aliponena nao wakaingia katika Uwepo Wake, walitambua ya kwamba walikuwa nje, hawakuwa—hawakuwa sawa, kulikuwa na kasoro fulani, kwa sababu walikuwa katika Uwepo wa Mungu. Naam. Nao wakasema, "Acha Musa aseme, wala si Mungu, kwa kuwa kama Mungu akisema sote tutakufa. Acha Musa aseme nasi."

²⁰ Ilikuwa katika Luka 5:8, ambapo wakati Petro...loo, wakati alipokuwa mtu mkuu mkaidi, na mtu mwenye ushawishi mkuu, nguvu nyingi ambazo tunafahamu. Yeye alikuwa kama mkatili, mvuvi mwenye sifa. Bali wakati alipouona mwujiza wa Mungu ukifanywa na Mtu wa kawaida, ilivyonekana, amba alitambua wakati huo ya kwamba huo ulihitaji zaidi ya mwanadamu kuwatupa hao samaki wote kwenye jarife ambapo yeye, pamoja na elimu yake yote, ujuzi wake wa kuvua samaki, alikuwa amevua usiku kucha wala hata hakupata kitu. Bali alimsikia Mtu Fulani akisema, "Litupe jarife lako ndani."

²¹ Na wakati alipoanza kuvuta, alikuwa na rundo kubwa la samaki, ndipo akatambua ya kwamba alikuwa mtu mwenye dhambi. Naye akasema, "Ondoka kwangu, Ee Bwana, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi." Ni nani aliyesema hivyo? Mtakatifu Petro, katika Uwepo wa Mungu, alimwombwa Mungu atoke mbele zake, kwa kuwa alijitambua kwamba ni mwenye dhambi.

²² Ibrahimu alijitambua "amekosea." Adamu alijitambua "amekosea," ambaye alikuwa ni mwana wa Mungu, alijitambua "amekosea." Musa alijitambua "amekosea." Israeli, kama kanisa na taifa, walijitambua "wamekosea." "Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi." Hakujaribu kusema, "Sasa, mimi ni mtakatifu na ninastahili kupokea jambo hili." Alisema, "Mimi ni mtu mwenye dhambi."

²³ Wakati mmoja mwanadini mmoja wa mtindo wa kikwaketekwae, pamoja na theolojia yote ambayo angeweza kujifunza chini ya mwalimu mashuhuri jina lake Gamalieli, jina lake lilikuwa ni Sauli wa Tarso, ambaye tunamfahamu kama Paulo, mwanadini kwelikweli. Aliifahamu dini yao yote ndani

na nje. Alikuwa ni Mfarisayo wa Mfarisayo, na Mwebrania wa Waembrania. Alikuwa ni mtu aliyesifika, msomi, mwerevu, mjanja, mwenye elimu, alidai alimjua Mungu tangu utotoni akikua. Lakini siku moja akienda zake Dameski, ile Nguzo ya Moto ilimulika juu yake naye akaanguka kwenye ninii yake... akaanguka miguuni mwake, ardhini, mavumbini, na kusema, "Bwana, ungetaka nifanye nini?" Mafunzo yake yote makuu, mafunzo yake yote makuu ya kitheolojia, elimu yake yote haikumaanisha kitu hapo aliposimama katika Uwepo wa Mungu.

²⁴ Ningetaka kusimama hapa kwa dakika moja na kusema ya kwamba hilo ndilo jambo lile lile. Huenda umepata DD., Ph.D., chochote ungeweza kuwa nacho, huenda umeenda kanisani tangu ulipokuwa mtoto, huenda umefanya matendo yote ya kidini yaliyoko, bali mara uingiapo katika Uwepo wa Mungu utajisikia duni sana na wala hu kitu wewe.

²⁵ Paulo alitambua ya kwamba alikuwa amekosea, naye akaanguka chini, chini ya ushawishi na Nguvu. Wakati alipoangalia juu na kumwona Mungu ye ye hasa aliyekuwa akimhubiri, na kumpinga, na aliyedhani alimfahamu, na akaona ya kwamba alikuwa amekosea, alianguka miguuni mwake, chini, kwa maana alikuwa katika Uwepo wa Mungu. Yeye alionna ile Nguzo ya Moto.

²⁶ Vipi kuhusu Yohana mkuu wa Ufunuo 1:7, wakati alipoonyeshwa lile ono, na akaangalia, na kusikia Sauti ikitisema naye. Ndipo akageuka aione hiyo Sauti, na akaona vinara saba vya taa. Na mmoja alisimama katikati ya vinara saba vya taa vya dhahabu, na nywele kama sufu, macho kama miali ya moto, miguu kama nguzo za shaba, Alikuwa amejifunga mshipi wa dhahabu kiunoni, na Yeye aliitwa Neno la Mungu. Na Yohana Mtakatifu mkuu akiisha kutembea pamoja na Kristo, aliegemea kifuani mwake, wakati alipofanya mambo haya yote! Kama nilivyosema asubuhi ya leo, huduma ya Paulo ilizidi ya kila mmoja wao. Hapa, Yohana akisha kutembea na Yesu, akaongea na Yeye, akalala pamoja na Yeye, akala pamoja na Yeye, lakini wakati alipomwona amesimama pale, hiyo hali ya kutukuzwa, alisema alianguka kama mtu aliyekufa miguuni Pake. Amina. Wazia jambo hilo!

²⁷ Tunaweza kuja kanisani na kunena na kumsifu Mungu, na kadhalika, bali, loo, ndugu, tutakapomwona akija, jambo fulani litakuwa ni tofauti miyoni mwetu! Tunaweza kuwazia tunatekeleza jukumu letu la kidini kwa kwenda kanisani na kutoa zaka zetu. Tunaweza kuwazia ya kwamba tunatii amri za kanisa na kukariri kanuni zote za imani, bali hebu wakati mmoja tumwangalie Yeye, kitu hicho chote kinabadilika kila mahali. Naam, ni hakika.

²⁸ Mtu huyu mashuhuri, Yohana Mtakatifu, mtu mashuhuri namna hiyo, Biblia ilisema katika Ufunuo 1:7, ya kwamba “alianguka kana kwamba ni mtu aliyekufa.” Baada ya miaka mitatu na nusu ya ushirika pamoja na Kristo, alikuwa ni mmoja wa waandishi wa zile Nyaraka, aliandika nyuma Yake, alikula pamoja na Yeye mezani, akalala pamoja na Yeye kitandani, na kushiriki pamoja na Yeye popote alipoenda, lakini wakati alipogeuka kumwona, hakuwa na uhai tena uliosalia ndani yake. Alianguka sakafuni kama mtu aliyekufa, ama chini. Vema.

²⁹ Tunamwona Isaya, katika Isaya 6:5, kama tulivyosoma sasa hivi, nabii huyu mkuu mwenye nguvu, ni mmoja wa manabii wakuu kabisa walioko katika Biblia. Kuna Vitabu sitini na sita vya Biblia; kuna milango sitini na sita katika Isaya. Isaya anaanza katika Mwanzo, katikati ya Isaya yeye analiingiza Agano Jipy, mwishoni mwa Isaya yeye anauingiza ule Utawala wa Miaka Elfu; ni Mwanzo tu hasa, Agano Jipy, na Ufunuo. Kikamilifu! Isaya alikuwa ni mmoja wa manabii wakuu. Lakini siku moja alikuwa ameegemea kwenye mkono wa yule mfalme mkuu Uzia, Uzia alikuwa ameondolewa kwake, naye alikuwa amehuzunika. Alikuwa ni jamaa mzuri sana, alikuwa ni mtu mzuri mwenye haki, kama mfalme huyo mwenye haki (mfalme mzuri) alimtambua kama mtu mtakatifu na kumweka hekaluni.

³⁰ Isaya aliona maono. Yeye alikuwa ni nabii. Isaya alihubiri Neno. Alikuwa ni mhudumu. Isaya alikuwa ni mtu mtakatifu. Lakini siku moja, akisimama hekaluni, aliona njozi naye akauna Utukufu wa Mungu. Aliwaona Malaika wenyewe mabawa juu ya nyuso Zao, mabawa juu ya miguu Yao, wakiruka kwa mabawa, wakisema kwa sauti kuu, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana Mungu Mwenye Nguvu!”

³¹ Nabii huyo alitambua yeye alikuwa si kitu. Akasema, “Ole wangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye midomo michafu.” Nabii, nabii mwenye nguvu kuliko wote katika Biblia, mmoja wao. “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, na ninaishi kati ya watu wenyewe midomo michafu. Ole wangu, kwa maana ninauona Utukufu wa Mungu.”

³² Na akasema, wakati Malaika huyo aliposema kwa sauti kuu, “nguzo za hekalu zilitikisika huku na huku.” Ndugu, hilo litakufanya . . . Si kwamba tu nguzo za hekalu zitatikisika, bali mbingu zote na nchi zitatikisika wakati Yeye atakapokuja tena. Milima itatoroka, na bahari itaondoka, na kusema kwa sauti kuu, “Tusitiri na uso wake Yeye aketiye juu ya Kiti cha Enzi.” Utakuwa ni wakati wa kutisha sana. Nakwambia, rafiki mwenye dhambi, afadhali uwe ukilichunguza hilo. Hiyo ni kweli.

³³ Sasa, Isaya alisema, “Ole wangu, mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wachafu. Nami ni ninii, watu hawa wana midomo michafu.”

³⁴ Sasa kumbukeni, kama watu watakatifu jinsi hiyo walijitambua wenyewe ni “wenye dhambi” katika Uwepo wa Mungu, mwenye dhambi na asiyemcha Mungu atafanya nini Siku hiyo? Watu watafanya nini wanaoketi mikutanoni? Watu watafanya nini ambao wamezunga Nguvu za Mungu, ambao wamesikia kuhesabu kinyumenyume kwenye Neno, ambao wamemwona Mungu akijidhihirisha Mwenyewe, na (bila tashwishi yoyote) kila Andiko likitimizwa, nao bado watajaribu kwenda Mbinguni bila ya kuzaliwa mara ya pili na kumpokea Roho Mtakatifu? Biblia ilisema, “Kama mwenye haki akiokoka kwa shida, mwenye dhambi na asiyemcha Mungu ataonekana wapi?” Tutasimama mahali pa namna gani kama tukimwona Mungu akijifunua Mwenyewe moja kwa moja mbele zetu, na kuuona Utukufu wa Mungu kama tu vile watu hao walivyouona, na watu wa namna hiyo walipiga kelele, manabii na watu wenye hekima ambao Neno limewekwa msingi juu yao? Kama wao walisema kwa sauti kuu, na kuanguka miguuni mwao, na kupaza sauti, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, uchafu,” itakuwaje basi kwa mtu huyo ambaye hata hatakiri dhambi zake? Itakuwaje kwa tineja mvulana ama msichana ambaye hatakiri dhambi zake? Itakuwaje kwa mtu huyo mwenye moyo mgumu ambaye anafikiri anajua zaidi juu ya uumbaji wa Mungu kuliko Mungu Mwenyewe anavyoujua? Itakuwaje kwa mtu huyo aliyeatumia maisha yake yote akijaribu kuikosoa Biblia? Jamaa huyo ataonekana wapi? Wazieni jambo hilo!

³⁵ Huu ni uinjilisti. Huu ndio wakati wa kuwatikisa watu. Huu ndio wakati ambao Mungu alisema kungekuja wakati, Yeye aliyutikisa Mlima Sinai wakati mmoja bali kutakuja kutikiswa tena, ambako Yeye “hatautikisa tu Mlima Sinai, bali Yeye angetikisa kila kitu kinachoweza kutikiswa.” Lakini uliona Maandiko hayo mengine? “Bali tunaupokea Ufalme usiowenza kutikiswa!” Haleluya! Kila kitu kinachoweza kutikiswa kitatikiswa. Mbingu zitatikisika. Nchi itatikisika. “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno hilo halitapita kamwe. Kwa kuwa juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda kamwe.” Kila kitu kinachoweza kutikiswa kitatikiswa. Bali tunaupokea Ufalme ambao ni Neno la Mungu Mwenyewe, Naye Mungu ni Neno Lake. Yeye hajitikisi. Amina! Loo, jamani! “Bali tunaupokea Ufalme usiowenza kutikiswa,” hautikisiki, alisema Paulo yule mwandishi Mwebrania.

³⁶ Mtu kama huyo na mwanadamu kama huyo, wakati kama huo na jinsi walivyojisikia! Sisi pia, sisi wenyewe, tumeuona Utukufu wa Mungu kama vile watu hawa walivyouona. Hakika. Tumeuona Utukufu wa Mungu kama vile Ibrahimu alivyouona. Tumeuona Utukufu wa Mungu kama vile Musa alivyouona, Nguzo ile ile ya Moto, Nguvu zile zile za Mungu, Kristo yule yule bila ku-... akijifunua Mwenyewe, akijionyesha Mwenyewe, akilidumisha Neno Lake katika siku ya mwisho.

Tunawezaje kuptitia hapa basi, na kuondoka na kulichukua juu-juu hivyo? Tunawezaje kutembea kuja hapo na kushikilia kanuni zetu na madhehebu, na tusilichukue Neno la Mungu? Itakuwaje kwetu Siku hiyo? Itakuwaje kwetu, wakati tumeuona Utukufu wa Mungu?

³⁷ Watu wengine watasimama kwa mbali na kulidhihaki, wengine watalicheka, wengine wataliita ushupavu wa dini, wengine wanaliita kusoma mawazo, wengine wanaliita Beelizebuli, wengine wataliita kitu kimoja ama kingine. Kama ilivyo methali ya kale, “Wapumbavu watatembea kwa viatu vya njumu mahali ambapo Malaika wanahofu kukanyaga.” Hiyo ni kweli. “Mpumbavu amesema moyoni mwake, ‘Hakuna Mungu.’” Wakati anapomwona Mungu akidhihirishwa kikamilifu kabisa na Neno Lake Mwenyewe (sio na kanuni ya imani; bali kwa Neno Lake), na halafu atembee moja kwa moja juu yake na kulidhihaki, yeye ni mpumbavu. Kwa sababu, ni, Mungu ni Neno, Naye Mungu amejifanya dhahiri kwake, naye ni “mpumbavu,” Biblia ilisema. Itakuwaje kwake wakati itakapombidi kusimama mahali hapo? Itakuwa—itakuwa ni jambo la kutisha sana kwa mtu huyo Siku hiyo, asiyemcha Mungu.

³⁸ Wenye dhambi waliotubu, hata hivyo, hawana hofu yoyote. Loo, la. Mwenye dhambi atakayetubu, yeye anajua ya kwamba kuna Dhabihu ilijojaa damu inayongojea, kusimama mahali pake. Hilo ndilo linalonipa faraja. Nimeuona Utukufu wa Mungu. Nimezihisi Nguvu Zake. Ninajua mguso wa mkono Wake. Ninajua mguso wa marudio Yake. Ninajua ya kwamba Yeye ni Mungu. Na ninajua nimepotea, bali yupo Mtu anayesimama pale kwa ajili yangu. Amina. Yupo Mmoja anayesimama pale na kusema, “Baba, weka uovu wake wote juu Yangu, kwa kuwa yeye alinitetea huko chini duniani.” Haleluya! Ndipo ninaenda kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, kwa ujasiri, nikiwa na neema moyoni mwangu, kujua sio kwa matendo mazuri, bali kwa rehema Zake nimeokolewa. Si yale ambayo ningaliweza kufanya, kile ningeweza kujiunga nacho, kile ningaliweza kusema; bali ni kwa neema yake ambapo aliniokoa mimi.

³⁹ Si ajabu yule mshairi aliyeshika hilo, alisema kwa sauti kuu, “Neema ya ajabu, ni sauti tamu jinsi gani, iliyomwokoa maskini kama mimi. Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, bali sasa nimepatikana; kipofu, bali sasa ninaona.”

⁴⁰ Ninawezaje kupata kwenda Mbininguni? Ungewezaje kwenda Mbininguni? Hatuwezi kwenda, sisi, wala hakuna njia ya sisi kwenda. Bali yupo Mmoja aliyefanya njia. Naye Ndiye Njia. Nasi tunafikaje Kwake? Kwa Roho mmoja, Roho Wake, tumebatizwa kuwa Mwili mmoja ambao utafufuliwa kama mzingo. Tutaondoka duniani kama wanaanga wa siku hii ya

mwisho katika imani ya Mungu. Amina. Hakika. Wenyе dhambi waliotubu haiwabidi kuwa na wasiwasi. Mtu fulani yuko pale mahali pao.

⁴¹ Loo, halafu baada ya sisi kuja katika Uwepo Wake sasa, nasi tunajua tumekuwa katika Uwepo Wake, tumemwona akifanya mambo aliyofanya alipokuwa hapa duniani. Unaujuaje ninii... Unaujuaje mzabibu unaouangalia? Kwa sababu ya tunda unalozaa. Unajuaje kanisa unalohudhuria? Kwa tunda linalozaa. Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

⁴² Sasa, tunaona Yeye kamwe hakutuagiza kwenda kuunda madhehebu. Kamwe hakutuagiza twende tukafanye kanuni za imani. Bali alituonya dhidi ya vitu kama hivyo. "Kwa maana ye yote atakayeondoa lolote Kwake au kuongeza lolote Kwake, huyo ataondolewa, sehemu yao, katika Kitabu cha Uzima." Unaona?

⁴³ Kwa hiyo, hatujaagizwa kufanya lolote ila kudumu na hilo Neno. Na kama mtu ametumwa na Mungu, yeye atadumu na Neno, kwa sababu Mungu anaweza tu kutuma kwa Neno Lake. Unaona? Unaona, Yeye hana budi kudumu na Neno Lake. Ndipo tunapokuja katika Uwepo Wake, mtu akija mara moja katika Uwepo wa Mungu, yeye anabadilishwa milele, kama kuna mabadiliko yoyote kwake. Sasa, wapo wale wangeweza kwenda katika Uwepo wa Mungu na wasiujali. Huyo hakukusudiwa Uzima. Lakini kama alichaguliwa tangu awali na Mungu, mara hatua hiyo ikipigwa, yeye anajua jambo hilo. Hiyo inashika moto.

⁴⁴ Mwangalie maskini yule kahaba kule chini Samaria siku ile, mwanamke huyo. Alikuwa katika hali mbaya kiakili na kimwili. Tunajua jambo hilo. Lakini mara alipoiona hiyo ishara ikifanywa, ya Masihi, alisema, "Tunajua Masihi yuaja kufanya jambo hili. Huna budi kuwa ni nabii Wake."

Akasema, "Mimi Ndimi huyo Masihi aliyeandikiwa atakuja."

⁴⁵ Alitambua jambo hilo. Kamwe hakuuliza swalı lingine zaidi. Alianza jukumu mara moja, kujua ya kwamba kama alikuwa amepata jambo hilo na akaja katika Uwepo wa Mungu, alikuwa anawajibika kumwambia mtu mwingine kuhusu jambo hilo. Haleluya! Kweli. Mtu ye yote anayekuja katika Uwepo wa Mungu anawajibika mbele za Mungu, tangu dakika hiyo na kuendelea, kumwambia mtu mwingine. Hebu mwangalie Ibrahim, mwangalie Musa, mwangalie Petro, mwangalie Paulo. Mara walipokuja katika Uwepo wa Mungu, walijitambua ni "wenye dhambi," na kuutia muhuri ushuhuda wao kwa maisha yao. Hebu mwangalie maskini mama huyo, asingeweza kukaa zaidi, alienda mjini na kuwaambia wanaume, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Yamkini huyu

siye yule Masihi?" Wasingeweza kukanusha jambo Hilo, kwa sababu likuwa ni la Kimaandiko. Hakika. Naam, hawana budi kufanya jambo hilo, mtu, wakati tukiwa na jukumu la kuwaambia wengine kama vile Musa alivyofanya, kama vile Petro alivyofanya, kama vile Paulo alivyofanya. Baada ya mambo haya, umeliona na ukaja katika Uwepo Wake, wewe unawajibika kwa Ujumbe kumfikia mtu mwingine. Kamwe huwezi tu kuketi kitako nao. Huna budi kumpelekeea mtu mwingine.

⁴⁶ Ninakumbuka dada mkongwe aliyekuwa hapa, mama yake Ndugu Graham Snelling, alikuwa akiti papa hapa kanisani, naye angeimba, "Ndiyo kwanza nipate ushindi! Ninakimbia mbio, mbio, mbio, nami ndio kwanza nipate ushindi wala siwezi kuketi chini." Alikuwa tu ndiyo kwanza apate kitu fulani. Nilienda kule kwenye kanisa dogo la watu weusi hapa Louisville, nao wote walikuwa wamesimama, wakiimba, "Ninakimbia kwenye Barabara Kuu ya Mfalme, nimeipata sasa hivi, ndipo nikakimbia kwenye hiyo Barabara Kuu!"

⁴⁷ Kuna kitu fulani kuhusu jambo hilo, unapompata Kristo, huwezi kujizua tena. Siku zako zilizosalia wewe ni mtu aliyebadilishwa, kwa kuwa wakati uhai na Uzima zinapoungana pamoja, hutoa Mwanga mkali. Kweli. Wakati glopu inapounganishwa na waya, kama ni glopu nzuri, haina budi kutoa mwanga; wakati umeme na balbu zinaposhikana, hakuna la kufanya ila kutawanya mwanga. Haina budi kufanya hivyo. Na wakati mwanamume ama mwanamke amechaguliwa tangu zamani kwa Uzima wa Milele, nao wanauona umeme wa Mungu ukiishika hiyo glopu, atatupa Mwanga popote awezapu. Wewe huenda usiwe ni wa zaidi ya wati kumi, bali utautawanya Mwanga ulio nao. Kama wewe si wa wati mia tano, tawanya Mwanga wa wati kumi. Toa Mwanga wako! "Nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuona matendo yenu mema na kumtukuza Baba aliye Mbinguni." Naam, bwana.

⁴⁸ Wakati mtu anapokutana na Mungu, anajitambua mwenyewe "si mwema." Mtu anawezaje kutembea huku na kujigamba jinsi alivyo mkubwa na yote aliyofanya, wakati yeze si kitu? Kwanza yeze si kitu. Siku moja huko chini Memphis, Tennessee, ama moja... Sidhani ilikuwa ni Memphis. Ilikuwa ni moja ya mahali hapo. Nilikuwa na Ndugu Davis na tulikuwa tuna u—uamsho. Huenda ilikuwa ni Memphis. Nasi tulikuwa, tulienda kwenye uwanja mkubwa wa michezo, nao kule ndani walikuwa na, si uwanja mkubwa wa michezo, ilikuwa ni namna ya nyumba ya sanaa, nao walikuwa na zile—zile sanamu kubwa walizokuwa wamepata kutoka sehemu mbalimbali za dunia, mbalimbali, Hercules na kadhalika, na wanasanaa mashuhuri walikuwa wamechora. Halafu walikuwa na uchanganuzi wa mtu aliyekuwa na uzito wa ratili mia moja na hamsini. Mnajua ni nini, thamani yake? Senti themanini na nne. Hiyo tu ndiyo

thamani yake. Senti themanini na nne ndizo kemikali zo—zote unazoweza kupata kwake. Ana chokaa ya kutosha tu kukinyunyizia kiota cha kuku, na ana za kutosha, kalisi kidogo tu, chumvi kidogo. Zote zingeuzwa kwa senti themanini na nne. Lakini tunashughulikia tu hizo senti themanini na nne na kuzibembeleza.

⁴⁹ Kulikuwako na wavulana wawili waliosimama pale, na mmoja akamwangalia huyo mwingine, kasema, “Jim, hatuna thamani kubwa sana sivyo?”

Akasema, “La, hatuna, John.”

⁵⁰ Nikasema, “Lakini ngojeni kidogo, enyi wavulana, mna nafsi mle ndani yenye thamani ya dunia elfu kumi, ambayo imeninii, inaweza kukombolewa na nguvu za Mungu, kama mtaiachilia tu.”

⁵¹ Mwanadamu, wakati anapoona mambo haya, ye ye anawajibika kuwaambia wengine. Niliona jambo hilo nilipokuwa tu mvulana. Niliyatumbia maisha yote katika jambo hilo. Ninasikitika tu nina uhai mmoja, laiti ningalikuwa na elfu kumi. Kama ningalikuwa na Umilele, ningali ningependa kuwaambia watu juu ya kitu hicho, maana ndicho kitu kikubwa sana nilichowahi kupata. Kama mtasoma katika Ezekieli 33, mlango wa 33 wa Ezekieli, kulikuwako na mlinzi aliyewekwa kwenye mnara, na mlinzi huyu alikuwa na jukumu juu ya mji mzima. Amina. Sasa, amkeni, jiamsheni dhamiri yenu ya kiroho kwa dakika moja, wakati nikilifungua Andiko hili. Mlinzi huyo ilibidi awe ni mtu aliyefunzwa. Ilimbidi kujua kile alichokuwa akifanya, kwa kuwa kwenye umbali wowote, mara walipotokea, adui, angeweza kumgundua. Angeweza kujua mwendo wao, angeweza kujua rangi yao, angeweza kujua cheo na safu yao. Kadiri macho ya mwanadamu yangeweza kuona, ye ye angeweza kumwona. Naye alikuwa juu kuliko hao wengine, kwa maana alikuwa amefunzwa kumjua adui. Na Mungu alimwajibisha mkononi mwake mji wote. “Mlinzi, habari gani za usiku?” Haleluya!

⁵² Hivyo ndivyo askari wa Mungu walivyo siku hizi. Wamefunzwa kwa Neno. Kitu chochote kinapotokea ambacho kimeng’arishwa kidogo, kilicho na kitu kingine mbali na Maandiko, wanaonya kusanyiko lao. Chochote ambacho si Biblia, chochote ambacho ha—hakifanani na Mungu, kama vile kufanya milo ya supu za jioni, madansi, na chochote kile, kuwalipa wachungaji. Mambo haya ni makosa. Michezo ya karata na tafrija za kadi makanisani, ni kosa! Basi mlinzi halisi aliye kuo ukutani, ambaye wakati mmoja amekwisha kuwa katika Uwepo wa Mungu... Kama hayuko juu ya ukuta, kama tu anapaswa kuwa juu ya ukuta, ukuta huo huenda usiwe mrefu kuliko kusanyiko. Bali kama ye ye ni mlinzi wa kweli, Mungu humwinua moja kwa moja katika milki ambazo hao wengine

kamwe hawazifiki. Bali analilinda kundi hilo, Na Mungu anamwajibisha kwalo! Mtu wa Mungu anayesimama Mbele za Mungu, na anajua Mungu ni Mungu, na anajua ya kwamba Mungu hulinda Neno Lake, na kumwangalia Mungu akitenda Mwenyewe na kutekeleza wajibu Wake na kudumisha Neno Lake, basi haidhuru ni mashirika mangapi ama madhehebu yanajaribu kulirarua, ye ye anajua cheo na safu ya adui. Amina. Anajua la kuliambia kusanyiko, mlinzi wa kweli.

⁵³ Kama tumekiri ya kwamba Yeye ndiye, tumekuwa katika Uwepo Wake, na tumetubu dhambi zetu, zimeondolewa kwenye kitabu cha kumbukumbu Lake. Hakuna mtu anayeweza kufanya jambo hilo ila Mungu. Sasa, unaweza kunifanyia jambo lolote, nitakusamehe, bali nitalikumbuka. Kama ningekufanyia jambo lolote, ungenisamehe, bali utalikumbuka. Bali Mungu anaweza kusamehe na kusahau hilo. Wazia jambo hilo, “hata halikumbuki!” Amina. Hilo linanifanya nijisikie vizuri. Wakati ambapo hata halikumbukwi tena, hakuna kitu kinachoweza kufanya hivyo ila Mungu. Hakuna kitu kinachoweza kufanya hivyo ila Mungu. Alisema angelifutilia mbali kutoka kwenye kitabu Chake cha kumbukumbu. Mimi siwezi kufanya hivyo, wewe huwezi kufanya, kwa sababu tuna hisi hizi ndogo tu zenye kikomo. Bali Yeye hana kikomo, Mungu, Yeye anaweza kusahau kabisa kwamba lilipata kufanywa kamwe. Amina.

⁵⁴ Msichana mmoja alitoka katika kanisa la mashambani, na baba yake alikuwa ni mhubiri wa mtindo wa kale, anayepiga makelele, ama mfuasi wa kanisa hilo. Na kwa hiyo msichana akahamia mjini, naye akachanganyikana kabisa na wanawake huko chini, na akaanza kutenda kama wao, na mitindo. Na kwa namna fulani siku moja aliwaonea baba na mama yake aibu kumtembelea, ama baba yake, hasa, mama yake alikuwa amekufa. Kwa hiyo mzee huyo, jambo pekee angalifanya, aliamka asubuhi, akala kiamshakinywa chake na kuichukua Biblia na kuisoma, na kulia na kuomba na kupaza sauti siku nzima, na kukimbia huku na huko chumbani, naye msichana kidogo alilionea hilo aibu. Kwa hiyo basi—basi wakati wote usiku kucha, kama aliishika Biblia, akaanza kuisoma, angeamka kitandani, na kupiga makelele, “Utukufu kwa Mungu! Haleluya! Loo, utukufu kwa Mungu!” Akacheza tu kwa kishindo na kulia nusu ya usiku.

⁵⁵ Kwa hiyo siku moja alikuwa awatumbuize wafuasi wake wa kanisa kwa karamu ndogo ya chai kama vile wanavyofanya sikuzote, mwajua, kwa hiyo hakujuu afanye nini na baba yake. Hata hivyo, alikuwa ni baba yake. Kwa hiyo akaamua angemweka juu darini, na kusema, “Baba, hutaki kuwa huku ambako wanawake hawa waliko, sivyo?”

Akasema, “La, siamini ninataka kufanya hivyo.”

⁵⁶ Akasema, “Vema, tutakuwa na wanawake wa kanisa hapa leo, nasi tutakuwa na mkutano mdogo, mkutano mdogo wa maombi. Kwa hiyo na—nakwambia, baba, mbona usipande tu uende darini?”

Kasema, “Ninaamini tu nitafanya hivyo.”

⁵⁷ Kwa hiyo akasema, “Soma kitabu hiki kizuri.” Ndipo akampa jiografia. Akamnyang’anya Biblia yake kusudi anyamaze. Kwa hiyo alijua kama angeisoma Biblia, mbona, angeanza kupiga kelele nyngi sana kule juu. Kwa hiyo yuko moja kwa moja juu yao, mwajua, mahali walipokuwa na karamu yao. Kwa hiyo akampa jiografia, kasema, “Hiki ni kizuri. Unapaswa kukisoma, baba, kwa sababu kinakwambia ukweli wote kuhusu ulimwengu.”

Vema, kasema, “Nitafurahi kukisoma hicho.”

⁵⁸ Kwa hiyo akasema, “Sasa wewe panda uende kule juu na unyamaze kabisa mpaka wanawake hawa watakapoondoka, na ndipo nitaninii... unaweza kushuka urudi huku na kufanya lolote unalotaka.” Akakubali kufanya hivyo. Kwa hiyo akaenda kwenye orofa ya juu, akaketi kule juu.

⁵⁹ Nao wote walikuwa wakifanya karamu yao ya chai, wajua, wakizungumza juu ya *nanii*, na mnajua jinsi yanavyoendelea, wakiwa na wakati huo wote mzuri. Basi mnamo wakati huo kitu fulani kikaachilia huko juu, kupiga makelele kote na kuruka, na plasta ikianguka. Mzee huyo akikimbia mbio huku na huko darini kwa nguvu alivyoweza, akiruka-ruka, na kupiga makelele, “Utukufu kwa Mungu! Utukufu kwa Mungu!” Hao wanawake hawakujua kile kilichotukia kule juu, kile walichokuwa nacho kwenye orofa ya juu. Kwa hiyo moja kwa moja akashuka kwenye vipandio, upesi alivyoweza.

Akasema, “Baba, nilikupa cha jiografia kusoma.”

⁶⁰ Akasema, “Naam, najua. Unajua,” kasema, “nilikuwa nikisoma katika jiografia hii hapa ambapo kuna mahali baharini ambapo hapana mwisho wake.” Kisha kasema, “Nilisoma hapa katika Biblia jana, Yeye alisema alizitupa dhambi zangu katika ‘bahari ya usahafulifu.’ Utukufu kwa Mungu...?...” Kasema, “Zingali zinashuka. Hazina mwisho, zinaendelea tu kushuka.” Hiyo ni kweli. Naye aliquwa akipaza sauti kuhusu jambo hilo. Vema, hiyo ni kweli.

⁶¹ Mungu huwiweka dhambi zetu katika bahari ya usahafulifu, anazifutilia mbali, nazo ziko kana kwamba kamwe hazikutendeka. Loo, jamani! Basi tunasimama kwa neema ya Mungu, kuititia Yesu Kristo Bwana wetu, safi na watakatifu, watakatifu tu kama alivyokuwa Yeye, kwa kuwa Yeye hanioni mimi ninapokuja huko juu, anamwona Mwanawewe Mwenyewe. Njia pekee anayoweza kuona... Hawezi kuniona, kwa kuwa nimo katika Mwanawewe. Naye anamwona tu Mwanawewe. Hilo

si ni la ajabu? Haitubidi kuwazia juu ya dhambi tena, zote zimekwisha, ziko chini ya Damu. Naam, bwana. Haitubidi kuwa na wasiwasi juu yake tena, zote zimetoka, na hazimo kwenye kumbukumbu la Mungu. Hata hazikumbuki tena.

⁶² Isaya, yule nabii mwenye nguvu, wakati alipozitubu dhambi zake, alisema, "Ole wangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye midomo michafu." Nabii! "Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, na kusanyiko langu ni chafu." Mnaona? "Watu ninaowahubiria, wao ni wachafu. Mimi ni mchafu. Na ole wangu. Lakini hili hapa kundi la Malaika linashuka kutoka kwenye Utukufu wa Mungu, likipeperusha ma—mawingu nyuma, nami ninaangalia kule juu na kuona pindo za vazi Lake likizijaza Mbingu zote. Nami ninawaangalia hawa Malaika ambao kamwe hawajapata kujuu dhambi ilikuwa ni kitu gani. Kamwe hawakujua dhambi ilikuwa ni nini, na hapo, wako Mbele za Mungu, wana mabawa mawili juu ya nyuso zao, wana mabawa mawili juu ya miguu yao, na wanaruka kwa mabawa mawili, na wanapiga makelele mchana na usiku, 'Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana Mungu.'" Whiu. Kwa namna fulani hiyo ingekufanya ujiskie mchafu, sivyo? Sasa, ye ye alifanya nini? Alisema, "Ole wangu."

⁶³ Basi hapo alipotubu dhambi zake na kusema "ole wangu," Malaika alienda kule na kuchukua koleo, akachukua kaa la moto ambalo lilimwakilisha Roho Mtakatifu na Moto, kisha akaja na kuliweka kwenye midomo ya nabii, na kusema, "Nimekutakasa." Ndipo mabawa yakipepea namna hiyo, yaliyaondosha mapazia ya wakati, naye akamsikia Mungu akisema, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?"

⁶⁴ Lakini baada ya kuona kwamba kulikuwako na njia ya kuiondoa dhambi, Mungu alitaka mtu fulani aende kwa ajili Yake, naye akasema, "Mimi hapa, nitume mimi." Alikuwa ameingia katika Uwepo wa Mungu, naye aliquwa amezitubu dhambi zake, na aliquwa ameoshwa dhambi zake, na aliquwa tayari kwa ajili ya huduma. Amina.

⁶⁵ Kama vile mshairi aliviyoshika hilo, kasema, "Mamilioni sasa wanakuwa katika dhambi na aibu, sikilizeni kilio chao cha huzuni na uchungu. Hima, ndugu, hima ukawaokoe; upesi jibu, 'Bwana, mimi hapa.'"

⁶⁶ Ninapowazia juu ya Afrika, India, na kote ulimwenguni, mamilioni ya makafiri wakipiga mayowe na kulia wapate rehemza, basi ni nani atakayekwenda? Sio kuwasambazia kitini, bali ni kuwalettea Yesu Kristo. Mtu fulani katika Uwepo Wake, kama vile Musa, ambaye angeshuka aende kule na kuwaonyesha ukombozi wa kweli. Si kuwafanya wajiunge na kanisa, ama kupeana mikono na kuwa na kanuni ya imani, bali kuleta ukombozi kwa nafsi zao; mtu fulani mzuri mcha Mungu. Naam, Isaya alitubu dhambi zake naye akatakaswa.

⁶⁷ Baada ya Yakobo kupigana miereka usiku kucha, katika kutubu dhambi zake, mnakumbuka mahali alipokuwa? Paliitwa Penieli, P-e-n-i-t-e-l-i, Penieli. Neno *Penieli*, katika Kiebrania, linamaanisha “uso wa Mwenyezi Mungu.” Yakobo, maskini yule mtu mwenye hila alikuwa amekimbia kote... jina lake lilikuwa ni *Yakobo*, ambalo linamaanisha “mdanganyifu,” yaani mwongo, alikuwa amekimbia maishani mwake mwote, mbali na Mungu, bali alipoenda wakati mmoja katika Uwepo wa Mungu huko Penieli, usoni pa Mungu, alimshika Mungu wala asingemwachilia. Mungu, tunahitaji Yakobo wengi zaidi. Yeye aliushikilia uso wa Mungu, katika Uwepo wa Mungu, alikaa mpaka jua likachomoza. Mungu akasema, “Niache niende, kwa maana jua linachomoza.” Naye alikaa usoni pa Mungu mpaka jua lilipochomoza, lakini aliondoka amehesabiwa haki na kuokolewa. Aha.

⁶⁸ Loo, jinsi liliyyokuwa ni jambo kuu, sasa, kujua ya kwamba alikuwa amepigana mwereka akashinda. Hiyo ni kusema, alikuwa ameziona ishara za Mungu, alikuwa ameota kuhusu Mungu, bali huu ndio wakati mmoja alipokuwa usoni pa Mungu, katika Uwepo wa Mungu. Wazieni jambo hilo, enyi marafiki. Sasa, tunapoharakisha. Katika Uwepo wa Mungu, mwanadamu anabadilishwa. Yakobo alibadilishwa. Sasa angeweza kutembea pamoja na Mungu. Naam, alikuwa ni mtu tofauti na vile alivyokuwa wakati alipopanda kwenda kule. Vita sasa vilikuwa vimekwisha. Naam, bwana. Naye akaanza kujenga madhabahu. Hakuwa amezoea kujenga madhabahu, mwajua. Lakini, nawaambia, unapokuja katika Uwepo wa Mungu, unataka kujenga madhabahu mahali fulani. Unataka kupata mahali fulani unapoweza kuombea. Alijenga madhabahu. Alitakaswa, na Mungu alikuwa ameshinda.

⁶⁹ Naye Yakobo alibadilishwa kutoka *Yakobo*, “mdanganyifu,” akawa *Israeli*, “mwana wa mfalme, aliye na mamlaka pamoja na Mungu.” Hayo ndiyo yaliyompata Yakobo. Yule mdanganyifu, mwongo, asiye na haki, mchafu, mdanganyifu, alimdanganya ndugu yake, akamwibia haki za mzaliwa wa kwanza, kama ilivyokuwa, kutoka kwa ndugu yake, akachukua maskini njia chafu ya kufanya jambo hilo, mdanganyifu sana. Alimdanganya baba mkwe wake. Akaweka vijiti vya mpopla na kuwafanya ndama wenye madoadoa, wakati ng’ombe wakiwa wamebeba mimba walipokuja pale, angalia jambo hilo, nao hao kondoo... angekiona kile kijiti cha madoadoa na kufanya ng’ombe wa madoadoa, kinawapa alama za kuzaliwa. Mdanganyifu, akimdanganya baba mkwe wake mwenyewe. Alimdanganya mama yake, akamdanganya baba yake, akamdanganya ndugu yake, lakini wakati alipoingia mara moja kwenye... Yeye alikuwa ni mwenye hila. Alikuwa akikimbia kila mahali alipoenda, sikuzote anamkimbia Mungu, alikuwa anamkimbia ndugu yake. Bali alipokuja katika Uwepo wa Mungu, alitambua

alikuwa ni mwenye dhambi. Alifanya nini? Alifanya nini? Aliona nafasi yake. Alikuwa amekutana na kitu ambacho hata hakuwazia habari zake hapo kabla, naye akakaa pale mpaka dhambi zote zilipoondolewa. Loo, jamani! Mungu alimleta katika Uwepo Wake Mwenyewe.

⁷⁰ Mungu hufanya njia ya kuwaleta watu katika Uwepo wao, ndipo wanafanya uamuza wao. Wengine wao wanamtoroka, wengine wanamkimbilia. Kama wamechaguliwa tangu asili kwa Uzima, wanaliamini, wanalishikilia. Kama hawakukusudiwa, wanajaribu kuondoka na kusema, "Hakuna kitu Hapo." Unaona? Na huyo ndiye jamaa aliyepotea. "Jamaa anayeitubu dhambi yake, atapata msamaha. Kama ukiificha dhambi yako, hutafanikiwa." La.

⁷¹ Kwa hiyo Yakobo wakati yeye, unajua, kesho yake alikutana na Esau ndugu yake. Hakuhitaji msaada wowote kutoka kwake wakati huo. Hakuhitaji jeshi lake. Alikuwa na shughuli ya kujenga madhabahu. Hakumwogopa Esau tena.

⁷² Zaburi 16:8, Daudi alisema, "Nimemweka Bwana mbele yangu daima." Hilo ni jambo jema la kufanya. Zaburi 16:8, "Nimemweka Bwana mbele yangu daima." Kwa hiyo, asingeweza kuchanganyikiwa na jambo hilo. Alitaka kuhisi Uwepo Wake, kwa hiyo Daudi akasema, "Nimemweka Bwana daima mbele za uso wangu. Sasa mimi, Daudi, nimemweka Bwana mbele ya uso wangu, daima niuhisi—niuhisi Uwepo wa Mungu." Hilo si lingekuwa ni somo zuri kwetu sisi sote usiku wa leo? Kumweka Bwana mbele ya uso wetu kusudi tuuhisi Uwepo Wake. Kumweka mbele. Kwa nini? Mweke wa kwanza, mbele yako. Kwa nini? Ndipo hutafanya dhambi wakati unapotambua ya kwamba uko katika Uwepo wa Mungu daima. Unapotambua ya kwamba Mungu yu karibu, utaangalia unalo sema.

⁷³ Mwanadamu, wakati anapowazia ya kwamba Mungu ameondoka, atalaani, atawatamani wanawake, atafanya... ataiba, atadanganya, atasema uongo. Atafanya jambo lolote hapo anapodhani ya kwamba Mungu hamwoni. Lakini hebu mlele katika Uwepo wa Mungu, ataacha jambo hilo sasa hivi. Unaona? Ndipo Daudi akasema, "Nimemweka Bwana mbele yangu daima." Hilo ni jambo jema. Si ajabu Mungu alisema yeye alikuwa mtu aliyeupendeza moyo Wake. Mwanadamu atafanya kila kitu wakati anapowazia ya kwamba Mungu hayupo karibu. Lakini anapotambua ya kwamba Mungu yuko karibu, je! ulipata kumwona mwenye dhambi? Hebu mcha Mungu amwendee, ataacha kulaani kwake, kama ana heshima yoyote. Unaona? Hatafanya mizaha michafu ambayo angalifanya. Unaona? Unaona, ataachana nayo, kwa kuwa anajua ya kwamba yuko katika Uwepo wa Mungu, maana Mungu huishi katika maskani ya watu Wake. Unaona?

⁷⁴ Baada ya Daudi kufanya hivi, yeye alisema, "Moyo wangu utafurahi," Laiti mngalisoma hiyo, Zaburi 16. "Moyo wangu utafurahi, na mwili wangu utatulia katika tumaini." Kwa nini? Moyo wangu utafurahi kwa kuwa nimemweka Mungu mbele yangu daima. "Na mwili wangu utatulia katika tumaini; kama nikifa, nitafufuliwa tena. Kwa kuwa hatamwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu, wala hataiacha nafsi Yake katika kuzimu." Unaona? Wakati Daudi alipomweka Mungu mbele yake, naye alijua ya kwamba daima alikuwa katika Uwepo wa Mungu. "Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu."

⁷⁵ Sasa sikilizeni, enyi kanisa, ninawapenda. Nami ninawatakeni mnisikilize sasa. Kama vile Ndugu McCullough alivyozea kusema, nitasema jambo fulani. Daima mweke Mungu mbele zako, wala usitende jambo lolote ambalo usingelitenda Mbele Zake, kwa maana Yeye anakuangalia. Unaona? Mungu amewazingira wale wamchao. Haninii... Anakaa papo hapo tu karibu na wewe. Naye anajua kila kitu unachofanya, nawe hunu budi kutambua jambo hilo. Unapoanza kusema uongo, usifanye hivyo, kumbuka, Mungu anakusikiliza. Kama ukianza kufanya uongo mdogo, usiufanye, Mungu anakuangalia. Ukianza kulichukua Jina Lake bure, usifanye hivyo, Mungu anakusikiliza. Ukianza kuvuta sigara, Yeye anakuangalia. Unaona? Ninii yake... Tulizoea kuimba wimbo, "Kote barabarani ya kwenda kwenye kituo cha kweli cha nafsi, lipo jicho linalokuangalia; kila hatua unayopiga, jicho hili kuu liko macho, lipo jicho linalokuangalia." Kumbuka, fanya kama Daudi, mweke Bwana daima mbele ya uso wako. Ndipo moyo wako utashangilia na mwili wako utatulia katika tumaini, kwa maana Yeye aliliahidhi hilo. Naam, bwana. Yeye alijua ya kwamba angefufufuka kwa sababu Mungu alikuwa ameahidi hivyo. Vema.

⁷⁶ Tunapokuja katika Uwepo Wake, tunabadilishwa, tusiwe tulivyokuwa tena. Angalieni kote katika nyakati, kwa watu wa kila aina, kwa mwanadamu. Mwangalie Ibrahimu. Mnasema, "Vema, maisha yaliyobadilika ni kwa ajili ya wahudumu peke yao." Loo, la. Maisha yaliyobadilika ni kwa ajili ya kila mtu. Unaona?

⁷⁷ Sasa, Ibrahimu alikuwa ni mkulima, lakini wakati alipoisikia Sauti ya Mungu ikitisema naye, na akalionia lile ono, alikuwa ni mtu aliyebadilika tangu wakati huo na kuendelea. Alijitenga na jamii yake, kutoka ukoo wake wote, na akatembea kama msafiri na mgeni, katika nchi ya kigeni, maishani mwake mwote, akiishi katika mahema, kwa sababu alikiri dhahiri kwamba alikuwa akiutafuta mji Ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni alikuwa ni Mungu. Alijua ya kwamba kulikuwako na Mungu, na kulikuwako na mji mahali fulani Ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni alikuwa ni Mungu. Hivyo ndivyo Waebrania 11 inavyotwambia, ya kwamba alikuwa akiutafuta

mji ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni alikuwa ni Mungu. Alikuwa ni mtu aliyebadilika, ingawa hakuwa kitu ila mkulima tu. Bali aliona ono naye akaja katika Uwepo wa Mungu, naye alikuwa ni mtu aliyebadilika tangu wakati huo na kuendelea.

⁷⁸ Musa, yeye alikuwa ni mchungaji, lakini alikuwa ni mtu aliyebadilika wakati alipokuja katika Uwepo wa Mungu. Alikuwa ni mwoga, alikuwa akimkimbia Farao, na jeshi zima likimfuata. Lakini akiwa na fimbo mkononi mwake, alirudi na kuliteka taifa zima. Unaona? Kwa nini? Alikuja katika Uwepo wa Mungu. Alikuwa ni mtu aliyebadilika, mchungaji.

⁷⁹ Petro, mvuvi, hakujuua kitu kuhusu kuvua samaki...ama hakujuua kitu kumhusu Mungu, labda jambo pekee alilojua lilikuwa ni jinsi ya kuvua samaki. Lakini alipokuja katika Uwepo wa Mungu, na kumwona Muumba mkuu Ambaye angeweza kuwaumba samaki, wakati alipomwambia ashushe nyavu zake avue samaki. Hapakuwapo na samaki wowote pale, alizivuta tu nyavu zake juu. Lakini akasema, "Kwa Neno Lako, Bwana. Ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, na kama ukiishusha...kama nikiushusha wavu, uliniambia nifanyi hivyo; kwa Neno Lako, kwa maana Wewe na Neno Lako ni mmoja, ninaushusha wavu." Ndipo wakati alipoanza kuuvuta, alisema, "Ondoka, Bwana, mimi ni mtu mwenye dhambi." Unaona, mvuvi, baada ya Petro kukutana na Kristo hakuwa vile vile tena. Yeye, baadaye, alikuwa mwaminifu sana kwa Mungu, alipewa funguo za Ufalme. Naam, bwana.

⁸⁰ Paulo, Mfarisayo wa mtindo wa kikwake, aliyeelimishwa na kufunzwa katika dini yote ya...iliyokuwako ulimwenguni siku hizo, mmoja wa wanachuoni wenyne sifa sana nchini. Bali wakati alipokuja mbele ya ile Nguzo ya Moto siku moja, yule Mungu aliyekuwa amemwudhi, bila kujuua. Yeye alikuwa ni Mfarisayo, hakuamini ya kwamba Mungu alikuwa Mwanadamu. Alijua ya kwamba Mungu alikuwa ni Nguzo ya Moto, iliwaongoza watu Wake kutoka Misri, ilikuwa pamoja nao kote safarini. Lakini wakati alipoiona Nguzo hii ya Moto, alianguka kifudifudi. Ndipo akasikia Sauti ikitesema, "Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "U Nani Wewe, Bwana?"

⁸¹ Akasema, "Mimi ni Yesu." Yeye alikuwa ni mtu, aliyesema, "Mmebatizwaje?" Aliishakuwa katika Uwepo wa Mungu. Alikuwa ni mtu aliyebadilika tangu wakati huo na kuendelea, alikuwa ameingia katika Uwepo wa Mungu. Humbadilisha mtu.

⁸² Charles G. Finney, mwanasheria, mwanasheria mashuhuri wa Philadelphia, bali wakati alipokuja katika Uwepo wa Mungu aliacha somo lake la uanasheria na akawa mhubiri mwenye nguvu sana taifa hili liliyepata kuwa naye.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... alikuwa ni mhubiri, kwa sababu siku moja alikuja katika Uwepo wa Mungu. Akawazia, mara moja, angeisomea huduma. Mnakijua kitabu

chake. Nina kitabu cha maisha yake. Alitoka akaenda kuomba. Alidhani alikuwa ni mhubiri. Alikuwa na shauku, kuwa alitaka kuhubiri, naye alikuwa na mahubiri machache angejaribu kuhubiri. Alitoka siku moja, nje ya ofisi yake, kuomba, akaingia msituni. Akaenda nyuma ya mti uliochakaa uliokuwa umeangushwa chini, ambapo angeenda kila alasiri. Mtu wa kidini sana, bali hakuamini Hilo.

Kulikuwako na wanawake wawili kanisani, walioendelea kusema, "Bw. Finney, tunaomba ya kwamba utampokea Roho Mtakatifu."

Akasema, "Ninaye Roho Mtakatifu." Kasema, "Mimi ni mhubiri."

⁸³ Kasema, "Bw. Finney, wewe ni mtu mashuhuri, nawe unalishikilia sana Neno, bali unamhitaji Roho Mtakatifu. Tunakuombea." Wanawake wa kupendeza.

⁸⁴ Kwa hiyo akaendelea, akaendelea. Kwa hiyo kila siku angeenda nyuma ya ofisi yake, bosi wake na wote kule alikofanya kazi, naye angetoka nje ya ofisi yake ya uwakili na kwenda huko kuomba. Basi siku moja alikuwa huko nje akiomba na akasikia tawi likivunjika. Alifikiri bosi wake alikuwa akija, akimtafuta. Akaruka juu upesi sana. Alikuwa akisema, "Bwana Mungu, ninakuamini." Ndipo tawi moja likavunjika, akafanya, "Mmmh! Mmmh! Mmmh!" akasimama na kusema, akaangalia kote, aone ni kitu gani kilicholivunja tawi. Na hapo ndipo alipoingia katika Uwepo wa Mungu. Alitambua ya kwamba tawi hilo lilivunjika kwa kusudi fulani. Akasimama pale, machozi yakinirika mashavuni mwake. Akasema, "Labda hao wanawake wanasema kweli. Ninaona aibu kwa mtu fulani kuniona nikizungumza na Mungu wangu, bali nadhani ni heshima kwa mtu fulani kuniona nikizungumza na bosi wangu. Bwana wangu ni mkuu mara ngapi kuliko bosi wangu!" Kasema, "Bwana, nisamehe na unijaze na Roho Mtakatifu," akaanza kupiga mayowe na kupaza sauti. Alikuwa katika Uwepo wa Mungu. Akakimbia katikati ya mji upesi sana akaingia ofisini mwake. Akapiga makelele sana hata ilimbidi kwenda nyuma ya mlango, kasema, "Bwana, nitakuletea fedheha. Nifiche hapa mpaka nitakapotoka kwenye mpagao huu." Kwa nini? Alikuwa ameingia katika Uwepo wa Mungu. Alikuwa ni mtu aliyebadilika. Mahubiri aliyokuwa akihubiri, alihubiri mahubiri yayo hayo na watu wakaja madhabahuni. Mnaona, alikwisha kuwa katika Uwepo wa Mungu.

⁸⁵ Moody, maskini mshona viatu, karibu hakujua ABC zake. Hiyo ni kweli. Sarufi yake ilikuwa mbaya. Siku moja mtu mmoja alimwambia, "Sarufi yako ni mbaya sana, Bw. Moody."

Akasema, "Lakini ninawaokoa watu nayo." Kwa hiyo . . .

⁸⁶ Siku moja magazeti, mhariri alianza kuandika gazeti. Alienda huko kuona jinsi ambavyo mtu huyu angeweza

kushikilia umati wa watu chini ya hali zozote, maskini mzee mdogo, mwenye upara, na kadhalika, na alikuwa na masharubu yamening'inia chini sana, kwa namna fulani mwenye kitambi, naye alikuwa ni mtu mwenye sura mbaya sana ukimwangalia. Kwa hiyo gazeti hili kweli liliandika makala yake, kasema, "Sioni ni kitu gani ulimwenguni ambacho mtu ye yeyote angeona katika Dwight Moody." Kasema, "Yeye ana sura mbaya, sauti yake inaalika, ana masharubu yaliyofikia kiunoni mwake, yeye ana upara kama boga." Kisha kasema, "Inawezekanaje ulimwenguni humu mtu ye yeyote aende kuona chochote katika Moody?"

⁸⁷ Kwa hiyo ilitokea meneja wa Moody alilionia, kasema, "Angalia, Bw. Moody, nitakusomea hili." Moody asingeweza kulisoma yeye mwenyewe. Kwa hiyo akasema, "Nitakusomea maoni ya mhariri." Naye akayaandika.

⁸⁸ Moody alitikisa tu bega lake, kasema, "Hasha, wao huja kumwona Kristo." Hivyo tu. Kwa nini? Yeye alikwisha kuwa katika Uwepo wa Mungu. Kutoka kwenye kutengeneza soli za viatu, watu wapate kuivilaa; yeye aliwalisha watu Injili ya maandalizi. Kwa nini? Yeye alikuwa katika Uwepo wa Mungu. Kweli.

⁸⁹ Maskini mwanamke mmoja wakati mmoja alikuja katika Uwepo wa Mungu, akiwa ni mwenye hatia alivyowenza kuwa. Mara moja wakati alipotambua ya kwamba alikuwa katika Uwepo wa Mungu, kila dhambi ilisamehewa naye alikuwa safi na mweupe kama yungiyungi. Loo, jamani. Ni watu wangapi zaidi ningaliweza kuwataja hapa, wakati usingeruhusu.

⁹⁰ Lakini ninataka kuzungumza kidogo juu yangu. Ni kitu gani kingaliweza kuwa duni kuliko mimi? Nilikuwa wapi? Nilitoka kwenye familia ya walevi, nilitoka kwenye familia ya wauaji, nilitoka kwenye familia ya wauza pombe haramu. Nanyi mnajua jambo hilo, kila mmoja wenu anajua jambo hilo, anajua ni jina la aina gani tulilokua nalo hapa. Watu hawakuzungumza nasi mtaani. Ningeenda mjini, nianze kuzungumza na mtu fulani, hakuna mtu angezungumza nami isipokuwa pasiwe na mtu mwingine karibu. Wangesema nami, mtu mwingine akaribie, wangeniacha. Nami ningesimama hapo na kulia, "La, hivi sivyo, haiwezekani. Hili halifai."

⁹¹ Lakini siku moja nikaja katika Uwepo wa Mungu. Akanibadilisha na kunifanya mwana wa aina nytingine. Neema Yake ilinileta katika Uwepo Wake. Kamwe sijatamani kuuacha. Nimekuwa humu ndani sasa kwa muda wa miaka thelathini na kitu. Sitaki kuuacha. Nina hakikisho ya kwamba daima nitakuwa Hapo. Hata mauti yenyewe kamwe haitanitenganisha na Uwepo Wake. La. Nitakuwa pamoja na Yeye milele. Nilipouona Uwepo Wake kwa mara ya kwanza, niiilia kama Isaya, "Ole Wangu." Ndipo akanigusa kwa neema Yake.

Nilikuwa mtu aliyebadilika. Maskini haini aliyekuwa akitoka hapa nje na kufanya yasiyofaa na kila kitu, alibadilishwa, na tangu wakati huo nimekuwa mtoto Wake. Tangu wakati huo, nimetamani kuyatoa maisha yangu yote kwa ajili ya huduma Yake, laiti tu ningalikuwa na maisha mengine elfu kumi kumpa Yeye. Haya yanazeeka sana sasa, miaka hamsini na mitatu imepita. Kama miaka thelathini na mitatu ya hiyo imekuwa, ama thelathini na miwili ya hiyo imekuwa katika Injili. Laiti ningalikuwa na mingine elfu moja ambayo ningaliweza kuitumia. Kwa nini? Wakati mara moja nilipoingia kwenye Uwepo Wake na kutambua ya kwamba kulikuwako na Mtu fulani aliywependaka, kulikuwako na Mtu fulani ambaye alinipenda wakati hakuna mwingine aliyenipenda, kulikuwako na Mtu fulani aliyenijali wakati hakuna mtu mwingine aliyenijali. Niliukumbatia msalaba Wake, nikauvuta kwangu, na mimi na Yeye tukawa mmoja basi. Na tangu wakati huo na kuendelea nimempenda. Yeye alikitia waa kifua changu na moyo wangu kwa Damu Yake, kwa kunigusa na kuzisamehe dhambi zangu, nami nina furaha usiku wa leo kuwa mmoja wa Wake. Sitamani kamwe kuuacha ulimwengu huu wa Roho, ingawa mjaribu mara nyangi amejaribu kunishawishi; bali mimi ni salama katika kibanda cha Mungu, na nina furaha katika upendo na neema Yake, nami ninaishi upande wa haleluya. Jamani! Inafanya moyo wangu kufurahi.

⁹² Ninampendekeza kwa kila mtu aliyechoka. Ninampendekeza kwako wewe usiye na matumaini. Wewe ambaye hujapata kuwa Uweponi Mwake, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kutubu dhambi zako na kutambua ya kwamba umekosea, na Mungu ana yule Malaika aliyechaguliwa usiku wa leo, anayeitwa Roho Mtakatifu, ambaye ataziondolea mbali dhambi zako zote. Ndipo utapaza sauti, “Bwana, mimi hapa, nitume mimi.” Ndipo utainua mikono yako juu na kuimba, “Nitamsifu! Nitamsifu! Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenyе dhambi. Mpeni utukufu, enyi watu wote, kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.” Ninampenda. Nanyi je? Kuishi katika Uwepo Wake!

⁹³ Nilikuja mimbarani hapa asubuhi ya leo, nikijisikia vibaya sana na mgonjwa sana kutoptana... Ni—nilikuwa huko chini Kentucky juma lililopita pamoja na marafiki wangu wasiri wanaoketi hapa. Kama ningalikaa kule chini kwa muda mrefu sana, wangeniua, hakika wangeniua, kwa wema, baadhi ya wapishi wazuri sana niliopata kujuua maishani mwangu. Na wakati nilipofikia kilele changu, tayari nimeshiba kabissa, “Ndugu Branham, hivi hutakula baadhi ya hiki?” Na ni kizuri sana, ninajaribu tu kukishindilia ndani. Nilishiba sana hata nisingweza kutembea. Ni—nisingweza kulala, nami ningeamka na kutembea-tembea kidogo. Na sikuwa nikijisikia vizuri sana wakati nilipofika hapa asubuhi ya leo. Bali

mara nilipoingia katika Uwepo Wake, hilo lilitosha. Hilo lilitosha, wote ilitoweka basi. Hiyo ni kweli. Loo, kuishi katika Uwepo Wake!

Nitamsifu, nitamsifu,
 Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
 ajili ya wenyе dhambi;
 Mpeni utukufu enyi watu wote,
 Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nitamsifu*—Mh.]

Kwa kuwa amefanya mengi sana kwangu.
 Amesamehe dhambi zangu,
 Na Damu Yake imeosha dhambi zangu.

Nitamsifu, nitamsifu,
 Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
 ajili ya wenyе dhambi;
 Mpeni utukufu enyi watu wote,
 Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

[Ndugu Branham anaaza kuvumisha *Nitamsifu*—Mh.]

⁹⁴ Sasa kama upo hapa ndani usiku wa leo... Nami ninajua Uwepo Wake upo hapa. Nikisimama pale ndani muda mfupi uliopita, kwa msichana mdogo wa Church of God, Roho Mtakatifu alinishukia wakati nilipokuwa nikimwombea mtoto huyo mdogo. Wazazi wake walikuwa wameshuka wakaja kutoka kwenye uwanja wa kambi wa Church of God wa Anderson. Naye msimamizi kule, akimjua mtoto huyo, madaktari walisema “angeweza...hana budi kufa mara moja, kwa lukemia.” Msichana huyo mdogo, anayependeza, akiwa katika hatua zake za mwisho sasa. Alirudi pale na akanipa mkono wake mdogo, wote ulikuwa umevimba, ukiwa umedungwa sindano na kadhalika, na umekuwa bluu. Nikamwangalia, nikaona ono. Wazazi wake walikuwa ndio kwanza wamesoma kitabu huko nje. Hawakujua lolote juu yake. Msimamizi mkuu huko kambini aliawambia, akawaambia wamlete mtoto huyo hapa chini. Walitaka kurudi wakati tutakapokuwa na ibada ya uponyaji. Nami nikasema, “Mleteni mtoto huyo sasa,” nilijisikia kuongozwa.

⁹⁵ Nilipokuwa nimesimama pale ndani, Roho Mtakatifu alirudi moja kwa moja nyuma na kuileta historia ya mtoto huyo. Akasimulia yote jinsi yalivyotukia, yale waliyokuwa wamefanya. Akafunua shauku ya msichana huyo mdogo, ilikuwa ni kuwa mcheza piano. Na mama huyo karibu apige mayowe. Na baba huyo akasema, “Huo ni ukweli wa Mungu.” Ameketi pale pale kwenye gari sasa akisikiliza haya, asingeweza kuingia, akiwa ameketi huko nje akisikiliza haya sasa.

⁹⁶ Kulitokea utaji mkubwa wa kivuli ulioning'inia juu ya mtoto huyo. Ndipo nikasema, "Shetani, umeshindwa." "Mungu, wewe huna upendeleo. Na kwa nguvu za kufufuka Kwako, na kama mtumishi Wako, ninamwondosha pepo huyu kutoka kwa mtoto huyo." Nuru kubwa angavu ilimulika juu yake, ilikuwa imekwisha. Amina. Aha? Hakika, Yeye anastahili sifa zote!

⁹⁷ Yeye anajua mambo yote. Anajua moyo wako. Nawe unajua kile unachowazia; Yeye anajua, pia. Iwapo kuna dhambi ndogo inayoning'inia juu yako usiku wa leo, nawe usingetaka kwenda katika Uwepo wa Mungu ukiwa na hiyo juu yako, waweza mara nyingine tena kuinua mkono wako na kusema, "Ndugu Branham, niombee, ninataka kuwa katika Uwepo Wake kwenye Siku ile, bila hatia." Mungu akubariki. Mikono mungi, Mungu anaiona. Katika Uwepo Wake. Sasa nitawaambia la kufanya. Sasa sikilizeni tu kwa makini. Fanya kama Daudi alivyofanya, mweke Bwana mbele yako sasa hivi. Mweke Bwana kati yako na dhambi hiyo, hata hiyo dhambi ikuzingayo iwe ni nini. Huenda ikawa ni kusema uongo, huenda ikawa ni kuiba, huenda ikawa ni mawazo machafu, huenda ikawa ni hasira, huenda ikawa ni kunywa pombe, huenda ikawa ni kuvuta sigara, huenda ikawa ni kuchenza kamari. Sijui ni nini. Huenda ikawa ni tamaa mbaya. Huenda ikawa ni chochote kile. Sijui ni nini. Chochote kile, mweke Bwana mbele zako. Na ndipo moyo wako utafurahi, na mwili wako utastarehe katika tumaini, kwa kuwa unajua ya kwamba Kristo aliahidi kufufua tena katika siku za mwisho. Atakapokuja, tutakuja katika sura Yake. Mbona usifanye hivyo wakati tukiomba.

⁹⁸ Baba yetu wa Mbinguni, Ujumbe mdogo uliokatakawta wa mtumishi aliyechoka. Lakini ninawazia tu juu ya somo la "kuishi Uweponi mwa Mungu." Nasi tunaona usiku wa leo matokeo yaliyoletwa juu ya watu watakatifu kuja katika Uwepo Wako, matokeo yake yaliyokuwa kwao. Watu wenye hekima, manabii wakuu na wenye nguvu waliochaguliwa na Mungu, na kutumwa wakalihubiri Neno, na hata hivyo walikutana Naye uso kwa uso na kuanguka chini kama mtu aliyeureka. Tutafanya nini kwenye siku hiyo, Bwana? Tumeliwazia. Tumekuwa tukiliwazia. Mikono kama arobaini ama hamsini imekuwa ikiliwazia, Bwana, kwa kuwa sasa hivi tu waliinua mikono hiyo, ama miyo chini ya mikono hiyo, imekuwa ikiwazia juu ya kukutana Naye tangu tumekuwa tukizungumza. Wangefanya nini kama iliwabidi kukutana na Yeye?

⁹⁹ Mikono yangu, Bwana, imeinuliwa. Nitafanya nini? Sasa, Baba, nina mambo mengi ninayokosea. Ndio kwanza nitibu dhambi yangu asubuhi ya leo mbele ya kanisa, kama nilivyoitibu Kwako juu ya mlima hivi majuzi asubuhi wakati upopo ulipokuwa ukivuma na theluji ikianguka, na kule juu ya mlima, jinsi nilivyolia na kukusihii unisamehe ujinga wangu. Na jinsi niliogopa sana kuja mbele ya ndugu zangu, ambao wengine

wao wanachukua kama nabii-mtumishi Wako. Na, Bwana, jinsi nilivyochukia kuja mbele yao na kuwaambia juu ya tendo la kipumbavu kwamba ningefanya kitu kama hicho, lakini, Mungu, ni jambo jema kwa nafsi yangu kwamba nitubu dhambi zangu wala nisizifiche. Kwa hiyo kuwa mwaminifu Kwako, na kuwa mkweli mbele ya watu, nimeitubia, Bwana. Nimekosea, nimekosea kabisa. Ninaomba msamaha.

¹⁰⁰ Ndipo basi, Baba, nimekuwa mzembe kukuhusu Wewe, kukutumikia, mara nyingi labda ningeenda muda mrefu zaidi wakati sikulifanya hivyo. Baba, natubu dhambi zangu. Ninataka Malaika wa Mungu anisafishe na hiyo, kwa Damu ya Yesu. Mikono mingine iliinuliwa usiku wa leo, baadhi yao huenda hawajapata kuomba msamaha hapo kabla; lakini nina hakika ya jambo hili moja, kama tutazitibu dhambi zetu, Mungu atazifutilia mbali, aziweke katika bahari ya usahaulifu na wala asizikumbuke te—tena. Na, Baba, ninapozitibu zangu, juu ya kutenda mabaya mbele ya watu hao, sikutenda kama mtumishi wa Kristo. Sikutenda. Nilihofu ya kwamba huenda watu wakanikasirikia na kufikiri sikutaka kumuudhi; bali sikuwazia yale niliyokuwa nikikufanya Wewe, Bwana. Na sasa na—naomba ya kwamba unisamehe. Na sasa, Baba, ninajua ya kwamba kama nikiomba msamaha ninapata msamaha, Nawe umeziweka katika bahari ya usahaulifu, wala hutaikumbuka hiyo tena. Mungu, ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo.

¹⁰¹ Pia naomba ya kwamba utamjalia kila mtu hapa, aliye na dhambi, dhambi izingayo ya chochote kile mbele yao, jalia waiondoe na kumweka Bwana mbele zao kama vile Daudi alivyofanya. Kwa kuwa sasa tunapaza sauti, “Ole wangu, kwa kuwa nimeuona Utukufu wa Mungu. Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, ama mwanamke au msichana mwenye midomo michafu, mvulana, ama yejete yule.” Chochote tunachoweza kuwa, sisi ni wachafu, nasi tunaomba Damu ya Yesu Kristo, ile Dhabihu ifaayo, itusafishe na dhambi zote, kusudi tupate kuishi katika Uwepo Wake. Jalia tuondoke hapa usiku wa leo huku miyo yetu ikifurahi, na miili yetu ikistarehe katika tumaini, tukijua jambo hili, ya kwamba Yesu akija, tutafufuka pamoja Naye katika sura Yake, nasi tutamlaki hewani, katika Unyakuo, wakati hatimaye kuhesabu kinyumenyume kutakapokwisha. Tunaona wakati wa saba wa kanisa tayari umehesabiwa ukaisha, nasi tuko tayari sasa kuondoka. Tunaomba, Mungu, ya kwamba Wewe, kabla hujaufunga mlango, kama kukiwako na mmoja hapa usiku wa leo ambaye hajapata kuingia, jalia waharakishe waingie upesi sana, kwa kuwa tunajisikia ya kwamba mlango wa rehema, kati ya rehema na hukumu, unafungwa. Wale watakaoikubali rehema wataingia. Wale ambao hawataingia itawabidi kupatilizwa hukumu. Mungu huufunga mlango. Jalia kusiweko na mlango utakaofungwa usiku wa leo kwa kila mmoja wa hawa wenye dhambi

wanaotubu. Jalia sote tupate msamaha na rehema. Katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁰² Na sasa, Baba, kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka, kwa wale ambaio ni wahitaji, ninaomba ya kwamba neema Yako itakidhi mahitaji yao yote. Jalia waingie katika Kristo, katika Uwepo Wake. Wamweke Kristo, Kristo, ile ahadi, “Alijeruhiwa kwa makosa yangu,’ hizo ni dhambi zangu. ‘Kwa mapigo Yake mimi nimeponywa,’ kwa hiyo ninamweka Bwana mbele ya ugonjwa wangu. ‘Yeye yuko upande wa mkono wangu wa kuume, wala sitatikisika,’ ndipo ninatembea kwa ujasiri, nikikiri ya kwamba nimeponywa. ‘Kwa mapigo Yake mimi nimeponywa.’” Tujalie, Bwana, kwa kila mmoja wao. Nasi tunajua ya kwamba kama tukitibu kwa mioyo yetu na, ama kwa midomo yetu, na kuamini ndani ya mioyo yetu, basi tunapata tunachotamani.

¹⁰³ Wewe ulisema, “Unaposema chochote, amini kitatimia, kitakuwa chako.” Tunaamini hilo, Baba, na tunaamini utatusafisha na dhambi zetu zote, na kuponya ugonjwa wetu wote, na utupe neema, Bwana, kukutumikia.

¹⁰⁴ Kuwa pamoja na watu hawa. Wengi wao watasafiri barabara zenye giza usiku wa leo. Wengi wao watasafiri maili nyingi. Usiache jambo lolote liwapate, Bwana. Wanakuja kutoka kote nchini kuketi hapa na kusikiliza kuhesabu kinyumenyume, kuona jinsi tulivyyokuwa karibu na wakati wa mwisho. Sasa nimewaomba waondoke, wakimweka Mungu mbele zao, daima mbele zao, mbele ya chochote kile. Mbele ya safari yao, mbele ya msogeo wao, mbele ya ninii yao—kabla hawajaamka, wakiisha kwenda kitandani, daima kabla hawajalala, popote pale, mweke Mungu kwanza! “Kwa kuwa yeye yuko kwenye mkono wangu wa kulia, wala sitatikisika.” Basi jalia mioyo yao ishangilie, kujua kwamba wamepata walichoomba, kwa sababu Mungu aliahidi, na miili yao itatulia katika tumaini. Tujalie, Bwana, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

¹⁰⁵ Sasa unaamini umemweka Bwana kati yako na dhambi yako, kati yako na ugonjwa wako, kati yako na kosa lako, kati yako na njia zako? “Bwana daima yuko mbele zangu, nami niko katika Uwepo Wake. Wakati mwingine nitakapoanza kuiwashaa sigara, Bwana yuko mbele yangu. Wakati mwingine nitakapoanza kutamani mabaya, Bwana yuko mbele yangu. Wakati mwingine nitakapoanza kusema lolote ovu, Bwana yuko mbele yangu. Wakati mwingine nitakapoanza kusema jambo baya, Bwana yuko mbele yangu. Nami sitatikisika. Amina. Nitaishi Uweponi Mwake kila siku, pamoa na shughuli zangu,

kila siku pamoja na maongezi yangu. Nitatembea kana kwamba Bwana yuko Mbele yangu, kwa sababu usiku wa leo nimemweka mbele yangu. Sitatikisika.” Je! mnampenda?

¹⁰⁶ Sasa, hebu na tusimame sasa. Loo, ninajisikia tu vizuri sana. Ninajisikia tu kana kwamba sitaki kwenda nyumbani. Nanyi mnajua zimesalia karibu tu dakika ishirini na tano ifike saa tatu, niko mapema karibu saa mbili. Hilo si ni la ajabu? Loo, jamani! Lakini sasa tunapoondoka, hebu na tukumbuke, hatuna budi kulipeleka Jina la Yesu, kama ngao dhidi ya kila mtego. Na wakati majaribio yanapotuzunguka... yakijaribu kutufanya tusikumbuke jambo hilo, taja tu Jina hilo takatifu katika maombi.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na majonzi;
Litakupa furaha na faraja,
Lo, lipeleke popote uendapo.

Jina la thamani (Jina la thamani), loo ni tamu
jinsi gani!

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani (Jina la thamani), loo ni tamu
jinsi gani!

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

¹⁰⁷ Ni wangapi wanaomfurahia mchungaji wetu, Ndugu Neville? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hivi hamna shukrani kwa Bwana kwa mtu mzuri, wa kawaida, mwaminifu, anayeiamini Injili? [“Amina.”] Naye anafanya kazi nzuri sana kwa kuzitii Amri za Mungu, na kulihubiri Neno na kudumisha hali hii nzuri sana ya kiroho kanisani wakati wote. Kumbukeni, nimeshuka kutoka Pwani ya Mashariki, nikapitia Kusini, na kupanda huko juu kwenye Pwani ya Magharibi, na kupitia Canada, wala sijakutana na kanisa moja ambalo ni la kiroho kama kanisa hili papa hapa. Yamepoa sana, naam, au ulokole, ama aidha yameingia katika hamaki, ama ni baridi sana hata hayawezi kutikiswa. Hivyo tu.

¹⁰⁸ Sasa, je! mnapendana mmoja na mwingine? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, peaneni mikono mmoja kwa mwingine, na kusema, “Bwana asifiwi.”

¹⁰⁹ [Ndugu Branham anapeana mikono na watu—Mh.] Bwana asifiwe. Bwana asifiwe. Bwana asifiwe, dada. Bwana asifiwe. Nina furaha ulikuwa hapa, ndugu. Bwana asifiwe, dada. Mungu akubariki. Vema. Mungu akubariki. Tutafanya hivyo. Mungu akubariki. Ninajua unachohitaji. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

Peleka Jina la Yesu,
Kama ngao dhidi ya kila mtego;
Majaribu yakikuzingira, (Unafanya nini?)
Taja Jina hilo takatifu katika maombi.

Jina la thamani (Jina la thamani), Loo ni tamu
 jinsi gani! (Loo ni tamu jinsi gani!)
 Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
 Jina la thamani (Jina la thamani), Loo ni tamu
 jinsi gani!
 Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

¹¹⁰ Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Kwa upole sana, hebu
 tusisahau hilo sasa. Hebu tuuimbe ubeti huo tena.

Peleka Jina la Yesu, (Kwa ajili gani?)
 Kwa ajili ya ngao dhidi ya kila mtego, (wakati
 Shetani anapojaribu kukutega);
 Majaribu yakikuzingira, (Unafanya nini?)
 Litaje tu Jina hilo takatifu.

“Kwa kuwa Bwana yuko mbele ya uso wangu; sitatikisika!”

Jina la thamani (Jina la thamani), Loo ni tamu
 jinsi gani!

Ndugu Neville.



KATIKA UWEPO WAKE SWA62-0909E
(In His Presence)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 9 Septemba, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwénye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org